JINA……..NAMBARI YAKO…….

TAREHE……

SHULE…… SAHIHI YA

MTAHINIWA……

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
LUGHA
MUDA: Saa 2½

MUUNGANO WA SHULE MBALIMBALI MTIHANI WA KUJITATHIMINI

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2

MAAGIZO

- Jibu maswali yote
- Majibu yako yaandikwe katika kijitabu cha maswali.
- Watahiniwa wanaweza kuadhibiwa ikiwa hawatafuata maagizo yaliyotolewa katika karatasi hii.

KWA MTAHINI PEKEE.

SWALI	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa kumi na mbili zilizopigwa chapa. Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

1. **SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Ajali haina kinga. Watu wengi wanapotajiwa neno ajali, fikra zao hukimbilia moja kwa

moja hadi barabarani. Mara chache mawazo yao huenda viwandani, mashambani au kwenye viwanja vya michezo. Ni nadra sana watu kufikiria kuwa nyumbani ndiko ajali nyingi zinatokea.

Idadi kubwa ya ajali nyumbani hutokea kimchezo tu. Watu wengi wameteleza msalani na wakapata majeraha mabaya. Wengine wameteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni, kama vile mafuta, mabaki ya chakula au hata maganda ya ndizi. Ulemavu walio nao watoto na hata watu wazima hutokana na ajali kama hizi wasizofikiria watu wengi.

Ajali vilevile hutokea watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba kuu ya kutenda. Katika hali hii, huweza kujiumiza au kuwaumiza wengine bila kujua. Hapa tunazungumzia watu ambao hujaribu kubeba mizigo yenye uzani wasiokadiria. Madhara huwa kuteguka viungo na kuchanika misuli.Aghalabu hulemewa na kubanwa. Mwandishi wa makala haya siku moja alipanda kibao kuangika picha ukutani. Ingawa alikuwa mfupi, ari ilimsukuma kuchuchumia. Matokeo ni kibao kilijisukuma nyuma. Mhusika alianguka akajigonga kidevu. Kitendo hiki kilisababisha yeye kujiuma ulimi vibaya, Kuvunjika jino na hata kuzirai. Bahati ni kuwa alikuwepo mtu aliyempa huduma ya kwanza na kumkimbiza hospitalini.

Hata hivyo ajali nyingi hutokana na vifaa vya nyumbani. Zana hizi ni pamoja na visu, meko ya gesi, mashine zinazotumia umeme na kadhalika na huwa hatari sana, hasa kwa watoto. Kitu kidogo hata kama wembe huweza kusababisha madhara makubwa. Kwa hakika hakuna yeyote kati yetu, hata waliokulia katika makasri ya fahari asiye na kovu. Makovu haya ambayo tunayaficha katika mavazi yetu ni ishara ya majeraha kutokana na ajali nyumbani. Je, una kovu lolote? Unakumbuka ulivyolipata?

Ingawa ajali hizi haziepukiki, yawezekana kuzipunguza. Ni muhimu kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani. Kwa mfano, ni hatari kuepua chungu chenye maji yanayotokota mekoni kwa mikono mitupu. Aidha ni kutowajibika kuchanganya kitu chochote chenye unyevu na mafuta moto mekoni. Watu wengi wamebambuka ngozi na nyumba kuteketea kwa namna hii. Kwa hivyo ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhakikisha tunavirudisha ipasavyo.

Jambo la tatu na muhimu zaidi ni kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa

huduma ya kwanza. Inawezekana kuokoa maisha au kupunguza majeraha kwa kuchukua hatua za dharura.

MASWALI

1. Eleza maana ya methali 'Ajali haina kinga! (alama2)

   .....

   .....

   .....

2. Kwa nini mwandishi anasema ajali nyumbani hutokea kimchezo? (alama3)

   .....

   .....

   .....

   .....

3. Ni mambo gani mengine yanayosababisha ajali nyumbani? (alama 3)

   .....

   .....

   .....

   .....

4. Onyesha vile inavyowezekana kupunguza ajali nyumbani. (alama 3)

   .....

   .....

   .....

5. Eleza maana ya :

   i) Jazba

      .....

      .....

   ii) Makasri

      .....

      .....

   iii) Makovu

      .....

      .....

iv) Kuepua

……

……

2. SEHEMU YA B: UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Dawa za kulevya zinaweza kugawika katika makundi mawili makuu: dawa hasi na dawa sugu. Katika kundi la kwanza zinaingia dawa zozote ambazo hunywewa, hunuswa au hutumiwa kwa nia ya kulevya au kumwingiza mtumiaji katika hali ya kujihisi amepanda'. Dawa za aina hii huwa na matokeo hasi kwenye mwili wa mtumiaji. Inawezekana jamii ikakubali kuwepo kwake, pamoja na kutumiwa kwake, lakini, matumizi ya kipindi kirefu huwa na matokeo mabaya sana kwa watumiaji. Baadhi ya dawa hizi ni bidhaa za tumbaku ambazo huwa na aina za kemikali inayoitwa nikotini. Nyingine ni vileo kama wiski, bia, divai, miraa au mairungi, gundi ya viatu na bidhaa zinazotokana na petroli.

Hebu sasa tuangalie zile zinazoitwa dawa sugu. Hizi ni dawa ambazo kimsingi humchangamsha mtumiaji na kumfanya apandwe na nishati za ajabu. Dawa hizi hufanya hivi kwa kuzitekenya seli za ubongo wa anayehusika. Katika kulifanya hili dawa zenyewe huishia kuzuia seli za ubongo huo. Huu ndio msingi wa mtumiaji kuwa na ustahimilivu fulani wa dawa zenyewe. Ustahimilivu huu ndio unaomfanya awe kama aliyetawaliwa na dawa hizo. Yaani mtumiaji huwa hana njia nyingine ya kujizuia na huishia kuwa mtumwa wa dawa hizo. Baadhi ya dawa sugu ni bangi, afyuni, heroini, mihadarati na kokeini. Baadhi ya wataalamu wanajumlisha miraa katika kundi hii pia. Ni kawaida kusikia madai kuwa mtu anayetumia dawa za kulevya huonekana kuwa na furaha kuliko wenzake. Ili kuelewa chanzo cha msisimko na furaha hiyo ya ajabu, lazima tuzijue hatua anazopitia mtumiaji dawa za kulevya. Kimsingi kuna hatua tatu kuu. Mara tu mtu anapozitumia dawa za kulevya, dawa hizo huzichangamsha seli za ubongo kwa kiasi kikubwa. Kuchangamshwa huku kwa seli kunazuia mwili wa anayehusika kutopata hisia kutoka viungo vya mwili au misuli ya mwili. Matokeo ya hali hii ni kumfanya mtu anyehusika kutenda mambo kupita kawaida yake. Mathalan, ataonekana kuwa na furaha nyingi, atasoma kupita kawaida, anaweza kucheza kwa kipindi kirefu na kadhalika. Hali hii inaweza kuitwa hali ya 'mpumbazo'. Mpumbazo huu unaweza kumdanganya anayehusika kuhisi kuwa ana uwezo usiokuwa wa

kawaida. Lakini hii ni hali ya muda tu ambayo hutangulia kuuliwa na kuharibiwa kwa seli za ubongo.

Mtumiaji anayeingia katika hatua ya pili huwa anatoka kwenye ile hali ya mpumbazo. Hatua ya pili hutambulishwa na dalili zifuatazo: Uchovu, kulala kupita kiasi, kutokuwa na hamu ya kazi au mambo mengine. Kupuuza maswala ya siha na afya, usahaulifu, kukosa malengo au shabaha katika kazi yake, kupungukiwa na kumbukumbu, kujitenga na watu wengine na kuwa na hisia za chuki au uhasama na jamaa. Mtumiaji anapofikia hatua hii hutambulikana waziwazi na watu walio karibu. Mtumiaji wa dawa za kulevya huweza tu kunusurika au kuokolewa katika hatua hii. Akipita hatua hii ya pili, huwa anaingia katika awamu mbaya sana.

Hatua ya tatu ya mtumiaji wa dawa za kulevya huitwa hatua 'isiyo ya kawaida'. Sifa za kutambulisha mtumiaji aliye kwenye ngazi hii ni fadhaa kubwa, unyonge wa mwili uiimbu wa kimawazo na uvunjifu mkubwa. Mtumiaji aliyefikia ngazi hii huonyesha sifa kadha milele. Mathalani kujitenga kabisa na jamaa au watu walio karibu naye, kupaliwa kabisa na usingizi, kuudhika haraka na kuwa na tabia ya kuonyesha uchukivu wa vitu kwa kupigana, kuchanganyikiwa kunakotokana na kuharibikiwa kwa seli za ubongo, wazimu au kuangukaanguka kama mgonjwa wa kifafa. Katika ngazi hii, seli za ubongo zinazomsaidia mtu kufanya uamuzi mzuri huwa zimeharibiwa na dawa zenyewe. Si ajabu basi kuwa mtumiaji anaonyesha tabia za kitoto na huishi kama mtu aliye kwenye ndoto. Hatimaye ubongo unazongwa kabisa kutokana na madhara ya seli na mtumiaji huweza kushikwa na magonjwa ya kiakili kama wendawazimu.

Mwisho wa mtumiaji wa dawa za kulevya aliyefikia ngazi hii ni kufariki baada ya mwili wake kushindwa kuhimili uzito wa dawa zenyewe. Wengine huishia kujinyonga au kufariki kutokana na madhara ya moyo.

MASWALI

a. Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (Maneno 45-50) (alama 7)

JARIBIO

……

……

……

……

……

.....

.....

.....

.....

.....

JIBU

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b. Eleza hatua anazopitia mtumiaji wa dawa za kulevya (maneno 90-100 (alama 8)

JARIBIO

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

JIBU

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Tunga sentensi moja ukitumia kitenzi - jina. (alama 1)

.....

.....

b) Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari (alama 2)

Kuchoka ndiko kulimfanya ajihami.

.....

.....

.....

……

c) Tumia neno nadhifu na nomino ya ngeli ya I-ZI katika sentensi kama ulivyoelekezwa. (alama 2)

i) Kivumishi

……

……

……

ii) Kielezi

……

……

……

d) Kanusha sentensi hii. (alama 1)

Mwanasiasa aliyeshindwa alitoka nje kwa hasira na kuuacha uchaguzi ukiendelea

……

……

……

e) Tumia mishale kuchanganua sentensi hii. (alama 4)

Nyanya anakunywa maziwa lakini mtoto anakunywa uji.

f) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo kwa kutumia T, Ts, na t (alama 2)

Mwakijana alikuwa akivaa polepole.

……

……

……

g) Eleza tofauti ya kimaana katika sentensi hizi (alama 2)

i) Nisimamapo huchekwa.

……

……

ii) Ninaposimama huchekwa

.....

.....

h) Tunga sentensi yenye kishazi huru na kishazi tegemezi na uviashirie (alama 2)

……

.....

.....

.....

i) Badilisha maneno yafuatayo ili yawe katika hali ya kuamuru (wingi) (alama 2)

i) Kuja

……

ii) Leta

……

j) Andika katika usemi wa taarifa (alama 1)

i) “Mama! Mama! Njoo uone ndege," mtoto aliita.

……

……

ii) Andika katika usemi halisi (alama 1)

Kiongozi wa nchi aliwashurutisha akina mama kugombea nafasi za kisiasa.

……

……

……

k) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 1)

N+V1+V2+T1+E+T2+N2

……

……

……

l) Kwa kuzingatia sehemu zilizopigiwa mstari, eleza maana ya sentenzi hizi (alama 2)

i) Milango ya nyanya ilifung<u>ama</u> alipoondoka.

……

……

ii) Mbona umejikunyata hivyo?

……

……

m) Babu ni mzazi wa kiume wa mama au baba.Babu pia ni: (alama 2)

……

……

……..……..

n) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya. (alama 2)

Mkembe, mkebe

……

……

……

o) Andika katika hali ya udogo. (alama 1)

Kijana yule alipewa kipande cha mkate na msichana mrembo.

……

……

……

p) Taja mifano ya sauti zifuatao (alama 2)

i) Kimadende

……

ii) Kitambaza

…..……

q) Tunga sentensi kisha ubainishe yambwa tendwa, yambwa tendewa na chagizo.

(alama 3)

……

……

……

……

r) Andika kinyume cha sentensi hii (alama 1)

Mtoto msichana alicheka kwa furaha.

……

……

s) Andika sentensi hii upya kwa kufuatia maagizo.

Nilikuwa nimejitayarisha vizuri kwa hivyo sikuona ugumu wowote katika safari yangu.

Anza:Safari

……

……..…

t) Toa maneno mengine yenye maana sawa na haya: (alama 2)

(i) Izara……

(ii) Anisi…….

u) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kuzingatia kauli zilizoandikwa kwenye mabano. (alama 2)

i) Watoto wamekunywa maziwa yote. (Tendwa)

……

……..

(ii) Yule mzee aliyemfanya msichana wake aolewe na mzee ameshtakiwa. (Kutendesha)

……

……

4. <u>ISIMUJAMII (ALAMA 10)</u>

a) Kuna nadharia tatu zinazohusu asili ya lugha ya Kiswahili. Zijadili huku ukionyesha kufaa au kutofaa kwake. (alama 6)

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

b) Eleza sifa za lugha ya taifa (alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……